For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**JINA______________________________________________NAMBARI**

**YAKO______________________**

**SHULE________________________________________________TAREHE___________**

_______________

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**
**LUGHA**
**JULAI/AGOSTI 2012**
**MUDA: 2 ½**

# MUUNGANO WA SHULE MBALIMBALI ZA WILAYA YA BUNGOMA
# MTIHANI WA KUJITATHIMINI 2012

KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
MUDA: SAA 2 ½

**MAAGIZO**

- Jibu maswali yote
- Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali
- Tumia hati safi

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Jumla | Tuzo |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| **JUMLA** | **80** | |



© BGM 2012 

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

***SWALI LA KWANZA: UFAHAMU***

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Ni dhahiri shahiri kwamba ***uharamia*** umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. .Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika na kanda ya Afrika Mashariki. Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi cha kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia na nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kuatiwa kwenye mizani.

Yamkini tatizo hili halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mjini Nairobi na Dare-es salaam mnamo Agosti 7,1998, na tukio la Septemba 11, mwaka wa 2001 kule Marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwingine, ukosefu wa tawala- wajibika katika maeneo kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati za kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umasikini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linalosawisishwa na 'kinyume mbele'. Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa kunaelekea kuzipiga jeki juhudi za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa, hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidhaa muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo wa malengo ya maendeleo ya milenia yanayosisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo na upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda mashariki ya bara la Afrika zimehujumiwa. Ni muhali kwa utali kustawi kwenye maeneo yaliyo na tishio la usalama. Itakumbukwa bayana kwamba watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za ***mtandao*** ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudi za maharamia katika



© BGM 2012 

bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni . Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyinginezo kwenye kanda ya mwambao zimetiliwa shaka si haba.

Itabidi mikakati kabambe na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa.

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**MASWALI**

a) Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwenguni? (alama 3)

__________________________________________________________________________________________________________________________________

b) Fafanua dhana ya "kinyume mbele," kwa mujibu wa taarifa hii. (alama 2)

__________________________________________________________________________________________________________________________________

c) Uharamia unaelekea kumtia hofu mwandishi. Fafanua (alama 3)

__________________________________________________________________________________________________________________________________

d) Thibitisha kuwa Kenya imeathirika pakubwa kutokana na vitendo vya uharamia. (alama 4)

__________________________________________________________________________________________________________________________________

e) Eleza maana ya msamiati huu jinsi ulivyotumiwa katika kifungu hiki. (alama 3)

i) Uharamia____________________________________________________________________

ii) Mtandao____________________________________________________________________

iii) Mwambao__________________________________________________________________

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

## SWALI LA PILI: MUHTASARI

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.***

Vijana wanapaswa waelewe umuhimu wa kurekebisha tabia. Hakuna haja ya kijana kufura kama kaimati anapoaswa. Mtu akikukanya jambo usichukulie kuwa hakupendi na wala usimfanyie kiburi kwani kufanya hivyo ni kinyume cha uungwana na utamkatisha tamaa mwenye kukurudi na akikuacha bila kukuonya utapata hasara na kukiona cha mtema kuni. Ni lazima wazazi wawaeleze watoto wao vile ambavyo walirekebishwa tabia zao zamani. Ifahamike kuwa wazazi walipewa adhabu kali kuliko hata zile wanazowapa watoto wao wa Ieo. Jambo la kushangaza ni kuwa ingawa waliadhibiwa hawakuwanunia wazazi wao bali waliwashukuru. Wazazi wengi wanadhani kuwa kufaulu kwao katika maisha kunahusiana sana na vile walivyofunzwa tabia nzuri. Wengi wanatoa shukrani kwa kuwatunza wakiwa hata wakongwe. Wanawapa heshima maalum ambayo si ajabu itakuwa nadra sana kupewa wakongwe wa miaka ijayo.

Binadamu gani anayekuwa bila kuonywa na bado awe mtu wa kuthaminiwa? Kama hata yai huguswa. sembuse wewe mtoto wa binadamu? Kwa nini usiguswe? Lazima uonywe hapa na pale, uadhibiwe inapopasa, ufokewe ukikosa au hata ukizidi uchapwe. Watu wote wanaohusika hasa wazazi na walimu yapasa wakuase wewe mtoto vilivyo mara unapopotoka bila kukudekeza. Pia unatakiwa uombe msamaha unapokosa na kuahidi kutofanya makosa tena.

Kijana asipoangaliwa ataweza kuzuzuliwa na ujana ambao mwenyewe hajui kuwa ni kama maua, huja na kwenda. kijana pia ni kama tembo la mnazi, huvuruga watu akili wakawa waongo, wenye dharau, wenye midomo michafu na nduma kuwili ambayo huleta zogo na zahama. Wengi huwa ni vitisho visivyo na mbele wala nyuma na wengine hawapendi kutumwa jambo kwa ugoigoi walio nao.

Badala ya kuwa washika adabu na washika dini, kuwa na bidii na wenye nyama ya ulimi. wao hukosa utu na kuharibu wakati wao kwa kutakiana matanga badala ya kuombeana heri. Vijana kama hao huwadharau wenzao wanaojitahidi kuwa wazuri na kusema ni mazumbukuku waliozubaa sana. Pia husema wenzao wanajigamba kwa wazazi na walimu ili wapendwe. Yote hayo ni kijicho, wanawaonea wivu kwa uzuri wao.

Vijana wanaodharauliwa namna hiyo husemekana kuwa ni mbumbumbu mzungu wa reli kwa kuzuiliwa tu Wasikate tamaa. Watie bidii kila mahali, wafaulu. Hao ndio watakaopata radhi za wazazi wao. Kwanza hufanikiwa sana maishani. huwa waadilifu na viongozi *bord* wa baadaye. Kule kusema sana kwa kuwa maarufu katika mambo ya kijinga sio kuendelea ni kujipoteza. Watoto wazuri hawazozani, huepuka

tandabelua za aina yoyote, hutulia kama maji mtungini. Yafaa ikumbukwe kuwa anayejitenga na maovu haingii hatiani. Waswahili hawakukosea walioposema kuwa aliye kando haangukiwi na mti.

Inatakiwa kijana ajiase na kujiuliza wapi ujana huo unamwelekeza na ukimtoka atakuwa ni mtu wa namna gani. Pia ajiulize kuwa uzee utamkuta akiwa amejijenga kitabia na kiuchumi ama atabaki akipiga malapa na kuwa kupe mjini. Ni vizuri pia ajue uhusiano wake na wazazi wake ulivyo na kuhakikisha kuwa ametenda ya kumfanya apate dhima ama ya kumfanya asionekane kama kibaparu tu.

Ingawa leo watu wanazidi kuamini kuwa mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, sikubaliani na msemo huo mara nyingi. Wakati mwingine si kweli. Kuna wakati inapofaa hata kusema mtoto umleavyo sivyo akuavyo. Labda umewahi kuona hapa na pale visa vya watoto walioleleka watoto wa viongozi wa dini na watoto wa wazazi wa kuheshimiwa ambao wameharibika. Labda wamekuwa hivyo kwa sababu ya umri, mazingira na kuchanganyika na marafiki wabaya. Watoto hao huzuzuka ghafula na kwa siri bila ya wazazi kujua na hata wakija kushtukia wanagundua kuwa watoto wameota sugu. Wazazi wanaweza kuwalea vizuri lakini matokeo ya malezi mara nyingi ni kama majaliwa tu. Watoto wote wanaweza kuwa wazuri lakini pakatokea mmoja kati yao wa kuleta kisirani akawa shetani kupindukia.

Wazazi huchukua hatua ya kuwakanya watoto wabaya lakini wengine hawasemeki. Mara nyingine huwapeleka hospitali wakiwadhani ni wagonjwa wa akili, ama, kutafuta marafiki wa kuwazungumzia lakini yote hayo hayafui dafu. Watoto hao watakuwa kama kitu cha kuvunda na hata uweke manukato gani uvundo hautaisha bali utahinikiza kila mahali. Wewe kama mzazi utaazirika lakini wao watajitia hamnazo na kukazana kufanya wayapendayo. Kwanza kama hao hawatambui juhudi za wazazi na badala yake wanawaona wazazi kama mashua ivushayo lakini mbovu.

Wewe kama mzazi ukipatwa na balaa kama hiyo utasemaje? Umeambulia patupu. Ungeleaje? Bila shaka utatindikwa na maarifa na labda utaamua umwache mtoto huyo kufunzwa na ulimwengu. Jambo utakalojifariji nalo ni kuwa hukumkosea huyo mtoto, umetimiza wajibu wako kama mzazi kwa kumkimu kwa kila hali, kumfunza elimu na dini ya kidunia na kwa kumpeleka shule ingawa kwa maajabu ya Firauni yamekupata hayo makubwa. Labda utabaki ukimuomba Mola muweza akakutengenezee ili mtoto apate kubadilika.

Kutumia mabavu katika kumrekebisha tabia ni kuzidi kumharibu kwani ni kama kumkunja samaki mkavu au kutarajia mazingaombwe. Mtoto amelilia wembe,

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

umemkanya hasikii basi utampa. Hakuna haja ya kuubanzabanza, wembe huo unaweza kukukata. Kweli uchungu wa mwana unao, lakini kung'ang'ania hivyo na mambo kama haya ni kujiumiza na kujiletea vidonda tumboni na kupata mvi za mapema mapema. Utakuwa unapiga ngumi ukutani. Katika hali kama hii wazazi wengine huamua kushika hamsini zao na kushughulikia mambo mengine yaliyo na maana zaidi.

kijana kama akiona umemwingilia sana atagura aende kutafuta atakaehokiita amani na furaha. Atauingilia ulimwengu kikuku. Huenda akataka kuishi mjini ambako atalifanya atakalo bila ushauri wa mtu yeyote, kwa kuwa kila mkuu wake ni tambara mbovu.

Mambo yanaweza kumwendea vizuri mwanzoni. Huenda akapata marafiki wa uongo na mashabiki vichwa maji kumshinda yeye hata mara kumi kwa ujuba wa kimji. Huenda kijana huyo akaona amefika kilele cha ufanisi na aishi maisha ya ufahari. Huenda akabadilisha marafiki na magari kama nguo. Huenda akasema anapendwa kupindukia na kuona kuwa wale wazumbukuku wa nyumbani watamchoka. Hayo yote si kitu, mji utakuja kumtoa ushamba.

Inawezekana siku moja kijana huyo asingiziwe jambo kubwa la kumfanya atiwe ndani baada ya urafiki wao wa kula na vivuli unapomalizika.Hapo labda atakimbiwa na marafikize na kujiingiza katika kisima alichojichimbia mwenyewe. Atagundua kuwa ulimwengu umemfunza. Wazazi pamoja na ndugu watakapopata habari zake watafunga safari mara moja kwenda kumwepua au kumwona. Watafanya hivyo si kwa kuwa walimtuma akatende maovu ila kwa kuwa damu ni nzito kuliko maji. Mtoto akiwaona hao wazazi na ndugu zake waliokuja kumwauni ataaibika na kujua kuwa kweli mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

**MASWALI**

a) Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno kati ya 50-55

**MAANDALIZI**



© BGM 2012

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**JIBU**

b) Mtoto umleavyo sivyo akuavyo.

Eleza kwa kutumia maneno kati ya 35 -40

**MAANDALIZI**

**JIBU**



© BGM 2012

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**SWALI LA TATU: MATUMIZI YA LUGHA**

a) Bainisha matumizi ya'ku' katika sentensi hii.

Kufaulu kwako kutakuletea heshima ikiwa hukudanganya katika mtihani huo. (alama 3)

b) Toa mifano miwili miwili kwa sauti zifuatazo: (alama 4)

i) Sauti ghuna ambazo ni vipasuo.

ii) Si ghuna ambazo ni vikwamizo.

c) i) Bainisha kielezi katika sentensi hii.

Wageni hao waliwasili Julai mwaka jana. (alama 2)

ii) Tumia viambishi viwili kama vielezi vya mahali katika sentensi. (alama 2)



© BGM 2012

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________

d) Virai vilivyopigiwa mstari katika sentensi ni vya aina gani. (alama2)

<u>Mwanafunzi stadi</u> <u>ndiye akayetuzwa.</u>

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________

e) Ainisha viambishi katika sentensi hii. (alama 2)

Mlipewa

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________

f) Tunga sentensi kwa kutumia vivumishi vifuatavyo.

i) Kivumishi cha kusisitiza. (alama 2)

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________

ii) Kivumishi cha a – unganifu.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________

g) Unda vitenzi kutokana na nomino hizi. (alama 2)

i) Hotuba______________________________________________________

______________________________________________________________

______________________

ii)

Tiba__________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________

h) Isahihishe sentensi hii.

Nilioyaona sitawai sahau maishani mwangu. (alama 3)

i) Eleza maana mbili zinazopatikana katika sentensi hii. (alama 2)

Huyu amekuja kutuliza.

j) Bainisha viwakilishi katika sentensi hii. (alama 3)

Aliwaletea kalamu tatu.

k) Andika katika usemi halisi

Waziri alisema kuwa wangepata tiba ya bure kama bunge lingepitisha msuada huo. (alama 2)

l) Bainisha vitenzi katika sentensi hii. (alama 3)

Juma ndiye aliyekuwa akiiba mifugo wa jirani.

m) Changanua sentensi hii kwa njia ya matawi.

Mwanajeshi mzee ambaye alijeruhiwa alipelekwa hospitalini. (alama 3)

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

n) Akifisha kifungu hiki. ( alama 3)

Wanyama hawa kiboko ndovu tembo ngiri na ngawa wanyama wa pori wote hupatikana katika mbuga ya maasai mara.

o) Tunga sentensi moja itakayodhihirisha maana mbili za neno 'kijinga' (alama 2)

**SWALI LA NNE: ISIMU JAMII**

a) Eleza maana ya mutilinguo. (alama 1)

b) Huku ukitoa mifano halisia eleza tofauti iliyopo kati ya kuchanganya ndimi/ msimbo na kubadili ndimi/msimbo. (alama 4)

c) Eleza sababu tano za kuchanganya na kubadili ndimi/msimbo. (alama 5)



© BGM 2012